




MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA

Na. 27 Toleo Maalum: Msimu wa Mvua Machi-Mei (MAM) 2021

Limetolewa 18 Februari, 2021

MUHTASARI

- Utabiri wa mvua za masika (Machi-Mei) 2021, ni mahususi kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka.
- Mvua za Masika zinatarijiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara pamoja na maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kakonko na Kibondo)
- Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarijiwa katika maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba.
- Mvua za Masika zinatarijiwa kuanza mapema katika wiki ya nne ya mwezi Februari, 2021 hususan katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini.
- Magonjwa ya mlipuko yanaweza kujitokeza kutokana na kutuama kwa maji machafu na uchafuzi wa maji safi.
- Vipindi vifupi vya mvua kubwa vinaweza kuambatana na mafuriko, maporomoko ya udongo na kusababisha uharibifu wa miundombinu, shughuli za kijamii kuathirika, upotevu wa maisha na mali.

MWELEKEO WA MIFUMO YA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MAM, 2021

Hali ya joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la kati la bahari ya Hindi na joto la juu ya wastani linatarajiwa kaskazini mwa bahari ya Hindi kwa kipindi cha msimu wa mvua za mwezi Machi hadi Mei (Masika) 2021. Joto la bahari la wastani katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kupunguza upepo wenye unyevunyevu unaovuma kutoka baharini kuelekea katika ukanda wa pwani. Aidha, joto la juu ya wastani kaskazini mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kusababisha upepo kuelekea katika eneo la pwani ya Somalia na hivyo kupunguza mvua katika baadhi ya maeneo ya pwani ya kaskazini. Katika msimu huu, kunatarajiwa kuwepo kwa matlai (upepo wa mashariki) katika maeneo mengi. Hali hii inatarajiwa kusababisha ongezeko la mvua katika maeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria na baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Aidha, vipindi vichache vya migandamizo midogo ya hewa katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi vinatarajiwa kujitokeza hususan katika miezi ya Machi na Aprili, 2021. Hali hiyo inatarajiwa kuvuta upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo na kusababisha ongezeko la mvua katika maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria na maeneo machache ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Aidha, katika eneo la kati la kitropiki la Bahari ya Pasifiki, joto la bahari linatarajiwa kuwa la chini ya

wastani hivyo kuwa na mchango mdogo katika mvua za Masika, 2021 hapa nchini.

MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA, MAM, 2021

Mvua za *masika* ni mahususi katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki, ukanda wa pwani ya mashariki na ukanda wa Ziwa Viktoria pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma. Maeneo haya yanapata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Kutokana na mifumo ya hali ya hewa ilivyo kwa sasa na inavyotarajiwa katika kipindi chote cha msimu kwa ujumla mvua za wastani zinatarijiwa katika maeneo mengi ya nchi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Hata hivyo, maeneo mengi ya nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa Ziwa Viktoria yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Aidha, maeneo ya pwani ya kaskazini yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Msimu wa mvua za Masika unatarajiwa kuambatana na vipindi vya mvua kubwa hususan katika kipindi cha mwezi Machi.

Kanda ya Ziwa Viktoria: (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kakonko na Kibondo)):

Mvua zinatarijiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi ya ukanda wa Ziwa Viktoria pamoja na kaskazini


mwa mkoa wa Kigoma. Mvua hizi zinataraajiwa kuanza katika wiki ya kwanza ya mwezi Machi, 2021 na kuisha katika wiki ya nne ya mwezi Mei, 2021.

Ukanda wa pwani ya kaskazini: (kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani (ikijumuisha visiwa vya Mafia), Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):

Mvua zinataraajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika maeneo mengi ya ukanda wa pwani ya kaskazini. Mvua katika maeneo haya zinataraajiwa kuanza mapema katika wiki ya nne ya mwezi Februari, 2021 na zinataraajiwa kuisha katika wiki ya tatu ya mwezi Mei, 2021.

Nyanda za juu kaskazini mashariki: (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):

Mvua zinataraajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi na zinataraajiwa kuanza mapema katika wiki ya nne ya mwezi Februari, 2021 na kuisha katika wiki ya tatu ya mwezi Mei, 2021.



Kielelezo: Mwelekeo wa mvua za Masika, 2021

ATHARI NA USHAURI

Sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Wanyamapori:

Katika kipindi cha Masika (Machi hadi Mei) 2021, hali ya unyevunyevu wa udongo kwa ustawi wa mazao na upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyama pori ikiwemo kilimo cha umwagiliaji vinatarajiwa kuwa vya kuridhisha katika maeneo mengi. Hata hivyo, mazao yanaweza kuathiriwa na hali ya unyevunyevu uliopitiliza, hivyo kuathiri ukuaji wa baadhi ya mazao yasiyohitaji maji mengi, kama vile mahindi, maharagwe na mazao ya mizizi. Mmomonyoko wa udongo, kupotea kwa rutuba na kutuama kwa maji mashambani, hususan kwa maeneo yanayotarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi juu ya wastani kunatarajiwa.

Aidha, katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani, upungufu wa unyevunyevu, maji na malisho kwa mifugo na wanyama pori unatarajiwa. Magonjwa ya mifugo yanaweza kujitokeza katika msimu huu wa mvua za Masika. Inashauriwa hatua za kuimarisha miundombinu ya ufugaji wa samaki hasa kwenye mabwawa zichukuliwe. Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu za ufugaji bora na uvunaji maji ya mvua na kuhifadhi malisho kwa ajili ya matumizi ya baadae. Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa pia kupata ushauri zaidi kutoka kwa wataalam wa kilimo, mifugo na uvuvi katika maeneo yao.

Sekta ya maji

Maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani yanatarajiwa kuwa na ongezeko la kina cha maji kwenye mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito. Hali hiyo inaweza kupelekea mito kufurika na kusababisha mafuriko katika maeneo ya mabondeni. Inashauriwa kutumia maji kwa uangalifu na kutumia mbinu bora za kuhifadhi maji kwa ajili ya matumizi ya baadae.

Menejimenti za Maafa

Mafuriko, uharibifu wa miundombinu, upotevu wa mali na maisha, milipuko ya magonjwa pamoja na athari nyingine zitokanazo na mvua nyingi zinaweza kujitokeza. Hivyo, mamlaka husika na kamati za maafa zinashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kuzuia na kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kutokana na vipindi vya mvua kubwa.

Zingatia

Mwelekeo wa mvua ulitolewa hapa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia taarifa za utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi na tahadhari kama zinavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.